OFISI YA RAIS – TAMISEMI
WIZARA YA ELIMU SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI
HALMASHAURI YA MJI MBINGA

SHULE YA SEKONDARI KINDIMBA,
S.L.P 62,
MBINGA

KUMB. Na. MOEVT/S.175/J.10/2

JINA LA MWANAFUNZI .....
SHULE ATOKAYO .....
S.L.P .....
MBINGA

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KINDIMBA HALMASHAURI YA MBINGA MJINI

1.0. Utangulizi
Nafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Kindimba ipo umbali wa kilometa kumi na tano (15km) Magharibi ya mji mkuu wa Halmashauri wa Mji wa Mbinga. Usafiri wa basi kutoka mjini Mbinga unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mbinga. Nauli ni shilingi elfu tatu (3,000/=)

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **20/01/2021**

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia
2.1.1. **Sare za shule**
Mwanafunzi ajapo shuleni aje na sare za shule zifuatazo

(a) Wasichana
(i) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
(ii) Sketi mbili nyeusi ziwe na urefu unaopita magoti
(iii) Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu
(iv) Sweta rangi ya Bluu lenye shingo ya V isiyo pasuliwa mbele
(v) Soksi nyeupe jozi mbili

(b) Wavulana
(i) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
(ii) Suruari mbili nyeusi ziwe za heshima siyo za **model** au **chupa (chini size 13)**
(iii) Jozi mbili za viatu vyeusi vya ngozi visivyo na kisigino kirefu
(iv) Sweta rangi ya Bluu lenye shingo ya V isiyo pasuliwa mbele
(v) Soksi nyeusi jozi mbili

2.1.2. **Sare za michezo**

- Wasichana
  - Bukta na sketi za rangi ya damu yam zee pamoja na T-shirt ya njano
  - Raba rangi yoyote
- Wavulana
  - Bukta rangi ya njano
  - T-shirt ya rangi ya njano yenye shingo ya V
  - Raba rangi yoyote

2.2. Pamoja na maagizo ya hapo juu unatakiwa kuja na vifaa utakavyotumia katika kusoma /kujifunza kwako. Vifaa hivi ni pamoja na

i. Daftari zisizopungua kumi aina ya Counter Book Q2 au zaidi
ii. Daftari kumi ndogo aina ya Msomi
iii. Kalamu za wino, penseli HB, rula na mkebe wa hesabu pamoja na
iv. Begi dogo la Madaftari

na vifaa vingine vinavyoweza kukusaidia katika kusoma/kujifunzia kwako.

2.3. Mzazi/Mlezi unatakiwa kumpatia mahitaji mengine muhimu ya kibinadamu mtoto wako kama vile fedha za matumizi (pocket money) n.k.

2.4 Shule haina bweni. Hivyo ikiwa mtoto anatoka mbali na shule angalau nje ya kijiji cha Kindimba mzazi unashauriwa kumtafutia mtoto makazi salama ikiwa ni chumba cha kulala na Chumba cha kusomea. Hakikisha mtoto wako unamtengenezea mazingira mazuri ya kujisomea ikiwa ni pamoja na kumwandalia kitanda, godoro, meza ya kusomea, ndoo ya kuogea, Shuka na Blanketi, pamoja na meza na kiti cha kusomea awapo nyumbani.

3.0 **MAJUKUMU YA SERIKALI**

i. Kununua vitabu, kemikali na vifaa vya maabara
ii. Ununuzi wa thamani na miundombinu
iii. Kugharamia elimu (Ada na michango)
iv. Madawati
v. Kugharamia shughuli za michezo
vi. Kukamilisha ujenzi na kukarabati miundombinu ya shule

3.1 MAJUKUMU YA MZAZI /MLEZI

- *Kuhakikisha kuwa huduma zifuatazo zinapatikana kwa wanafunzi:-*
  i. Sare za shule na michezo (itakua mali ya mwanafunzi mwenyewe)
  ii. Vifaa vya kujifunza vikiwemo daftari na kalamu
  iii. Chakula kwa wanafunzi wa kutwa
  iv. Matibabu (kila mzazi/mlezi ahakikishe kwamba mwanafunnzi ana kadi ya BIMA YA AFYA (NHIF) CHF. Huduma hii inapatikana katika kituo cha Afya cha Kindimba. Njoo katika kituo hiki upate maelekezo
  v. Mahitaji mengine ya kibinadamu kwa wasichana na wavulana kama vile magodoro, shuka na mito
  vi. Hakutakuwa na **HUDUMA YA BWENI KWA WANAFUNZI.**

4.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978, na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b. Kuwahi kufika shuleni na kuwa mstarini saa 1:00 asubuhi
c. Kuhudhuria shuleni siku zote na muda wote wa masomo
d. Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa ikiwemo vipindi vya dini kila wiki
e. Kuhudhuria kazi zote za mikono
f. Kuhudhuria mikutano ya shule mfano, Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha bendera ya Taifa, vipindi vyote vya masomo darasani, na vikundi mbalimbali vinavyotambulika kisheria mfano, vilabu vya masomo, dini utamaduni, maadili n.k
g. Kuitika miito ya dharura mara moja
h. Kushiriki kuimba wimbo wa taifa (wakati wa kupandisha Bendera), wimbo wa shule kwa siku maalumu iliyopangwa.
i. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
j. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
k. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
l. Kutunza mali ya umma (NB: ukiharibu utagharimia)

4.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule
(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli na kadhalika
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa maksudi mali ya umma
(g) Kudharau Bendera ya Taifa
(h) Kuwa mjamzito /kupata mimba
(i) Kuoa au kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa na simu ya mkononi

5.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi ni:-
(a) Medical Examination form ijazwe na Mganga mkuu wa hospital ya serikali (Hospitali ya wilaya ya Mbinga/**Mbuyula**) na ukabidhi kwa mkuu wa shule

siku ya kuripoti. Zingatia fomu za afya zisijazwe kwenye kituo cha afya, zahanati au hospitali yoyote za misheni mfano **Litembo, Peramiho Au Hospitali Ya Masista Mbinga fomu isiyojazwa kwenye hospitali ya wilaya/Mbuyula na kusainiwa na mganga mkuu itakuwa batili na haitapokelewa**

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kuto shiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

(c) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

Fomu zote hizi utakabidhi kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti zikiwa zimekamilika (zimejazwa) kikamilifu.

6.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

NB: Shule haitavumilia mwanafunzi atakayekiuka kanuni hizo hapo juu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
MKUU WA SHULE